



TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Magavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Prof. Florens Luoga, na Benki Kuu ya Zambia, Dkt. Denny Kalyalya, wanatarajia kutia saini makubaliano ya kuruhusu matumizi ya fedha za nchi mbili za Tanzania-Shilingi na ile ya Zambia-Kwacha katika kufanya biashara na uwekezaji katika miji ya mpakani ya Tunduma na Nakonde.

Makubaliano hayo yatatiwa saini huko Tunduma mkoani Songwe tarehe 21 Septemba 2018 mbele ya mgeni rasmi Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemas Elias Mwangela. Tukio hili litafuatiwa na mukutano wa hadhara.

Lengo la makubaliano hayo ni kuwezesha kupokelewa sarafu za nchi hizi mbili na taasisi rasmi za fedha ikiwa ni pamoja na mabenki ya biashara ya pande zote mbili bila kikwazo chochote. Nia ya hatua hii ni kurahisisha biashara kati ya nchi hizi mbili, kuondoa biashara holela ya fedha za kigeni mpakani na kuziwezesha serikali za Tanzania na Zambia kujipatia mapato stahiki ya kodi na tozo kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazofanyika katika miji hiyo.

Benki Kuu za mataifa haya mawili rafiki, zimefikia hatua ya kusaini makubaliano hayo baada ya utafiti na majadiliano yaliyoanza tangu mwaka jana ambayo yalikuwa na lengo la kupambana na biashara holela ya fedha za kigeni na kuwawezesha wananchi wa pande zote kunufaika na shughuli za kiuchumi za mpakani.

Aidha, makubaliano hayo yatasaidia kuleta ushindani wa haki kwa taasisi za fedha (mabenki na maduka ya kubadilisha fedha za kigeni) katika biashara na kuziwezesha Benki Kuu zetu kusimamia ipasavyo ujazi wa fedha katika soko.

Wananchi wa Tanzania na Zambia wamekuwa wakishirikiana katika nyanja mbalimbali kwa miaka mingei. Ushirikiano huu uliimariswa zaidi na viongozi waasisi wa mataifa haya, Dkt. Kenneth Kaunda na Hayati Mwalimu Julius Nyerere kwa kuanzisha reli ya pamoja ya TAZARA, bomba la mafuta la TAZAMA, harakati za ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika pamoja na masuala mengine mengi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Viongozi wa sasa wa serikali zote mbili, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Edgar Lungu, Rais wa Zambia wanaimarisha na kuendeleza ushirikiano huo. Hatua za utiaji saini wa makubaliano hayo unatarajiwa kuongeza hamasa kwa wananchi na taasisi mbalimbali kufanya shughuli za kiuchumi ili kujiletea maendeleo na kuchangia maendeleo ya mataifa haya mawili.

BENKI KUU YA TANZANIA
Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki
botcommunications@bot.go.tz
18 Septemba, 2018